**TAMKO KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU VITENDO VYA KIKATILI WALIVYOFANYIWA WATUHUMIWA WATANO HUKO LOLIONDO,**

**MKOANI ARUSHA**

## Utangulizi

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu Tanzania (LHRC) pamoja na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), kwa pamoja tunalaani vikali ukatili uliofanywa na Maofisa wa Jeshi la Polisi wilayani Ngorongoro dhidi ya watuhumiwa watano walioshikiliwa na jeshi hilo kwa muda wa siku 15 (kuanzia tarehe 21 Desemba 2018 hadi tarehe 4 Januari 2019) bila dhamana au kufikishwa mahakamani. Tatizo hili limekuwa sugu nchini kote, na leo tunatangaza pia operesheni maalum ya "Tetea Haki za Mtuhumiwa" kwa nchi nzima tukianzia na hili la Loliondo. Tunampongeza na kuamua kuungana na Waziri wa Mambo ya Ndani katika kutetea na kulinda haki za watuhumiwa nchini.

## Ukatili uliofanywa dhidi ya watuhumiwa

Mnamo tarehe 21 Disemba 2018, wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro wapatao watano kwa majina ya Peter Orkery, Musa Yahya, Kayanda Kisoki, Zakaria na Francis Arusha walikamatwa na polisi wilayani Ngorongoro na kushikiliwa kwa muda wa siku kumi na tano. Wananchi hawa wa jamii ya kimasai

wanatuhumiwa kuiba katika kampuni ya **Simba B** inayojishughulisha na utalii wilayani Ngorongoro ambapo baadhi yao wanafanyia kazi.

Siku ya kukamatwa kwao, polisi waliwachukua watuhumiwa hao kwa ajili ya kutoa maelezo, walipofikishwa kituoni walifungwa kamba mikononi na miguuni kisha wakatundikwa juu na kuanza kupigwa hadi miguu kupasuka. Baada ya mahojiano nao watuhumiwa hao wanadai pia kufanyiwa ukatili wa kutisha kwa kuingiziwa rungu za polisi na chupa sehemu za haja kubwa. Kwa sasa hali zao ni mbaya na wengine bado wanauguza majeraha yaliyotokana na vipigo na ukatili waliofanyiwa na askari wa Jeshi la Polisi Loliondo.

Baada ya kukamatwa tarehe 21 Disemba na kukaa mahabusu kwa siku 15, bila kuonana hata na ndugu zao, miguu ya baadhi ya watuhumiwa hao ilianza kuoza ndipo wakapelekwa mahakamani tarehe 4 Januari 2019. Baada ya hapo wote walilazwa hospitali ya Wasso kwa ajili ya matibabu. Watuhumiwa walifanyiwa upasuaji kwenye miguu na kutolewa usaha uliokuwemo katika miguu yao.

**Vitendo vya Polisi Kukiuka Haki za Watuhumiwa na Wananchi Loliondo na Maeneo Mengine Nchini.**

Ikumbukwe kuwa Jeshi la Polisi nchini limeanzishwa na linatakiwa kufanya kazi kulingana na sheria na miongozo mbalimbali iliyowekwa nchini. Pamoja na sheria zingine Jeshi la Polisi linaongozwa na *Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi* Sura ya 322 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2010. Katika Kifungu cha 5(1), sheria hiyo inatamka kuwa jeshi hilo limeundwa nchini kwa ajili ya kulinda amani, kusimamia sheria, kuzuia na kugundua uhalifu, kukamata wahalifu, na kulinda mali.

Katika kuzuia uhalifu, kukamata na kuwaweka kizuizini waalifu, Jeshi la polisi linapaswa kuongozwa na *Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai* ya mwaka 1985. Kwa mujibu wa sheria hiyo, mtuhumiwa anapokamatwa anakuwa na haki mbalimbali ikiwa ni pamoja na;

- kuambiwa kosa analotuhumiwa nalo,
- kupewa dhamana, kuonana na ndugu,
- kupatiwa matibabu
- kuhojiwa bila shuruti
- kuhojiwa mbele ya mwanasheria
- kuonana na ndugu
- kupelekwa mahakamani kwa wakati pamoja na
- kuelezwa haki yake ya kupata msaada wa kisheria.
- Kukaa mahabusu muda usiozidi masaa 24
- Kupewa dhamana ya polisi muda wowote hata siku za jumamosi na jumapili
- Kulala mahali salama na safi
- Kutokupigwa au kufanyiwa ukatili wowote
- Kutendewa kibinadamu na kujali utu

Katika hali iliyoanza kuwa ni ya kawaida kwa jeshi la polisi na vyombo vingine vya usalama, tumeshuhudia jeshi la polisi katika wilaya ya Ngorongoro na kwingineko nchini wakivunja haki hizi za watuhumiwa ikiwa ni pamoja na kukaa na watuhumiwa kwa muda mrefu kupita kiasi jambo ambalo ni kinyume na Kifungu cha 64(1)(c) cha *Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai* ya mwaka 1985 ambayo inaelekeza polisi kuwaweka kizuizini watuhumiwa kwa masaa yasiyozidi 24 kabla ya kuwapa dhamana au kuwapeleka mahakamani kwa mujibu wa sheria.

Kifungu cha 64(1)(c) kinaweza kutafsiriwa kwa tafsiri isiyo rasmi kama ifuatavyo:

> *"64(1)Bila kuathiri vipengele vilivyomo katika sheria nyingine zinazoongoza masuala ya dhamana ya Polisi, mtuhumiwa atakayewekwa chini ya ulinzi wa ofisa wa polisi kutokana na tuhuma za kufanya kosa la jinai ataachiwa mara moja ikiwa:*

*(c) Baada ya masaa ishirini na nne tangu mtuhumiwa kukamatwa, hakuna hati ya mashtaka iliyoletwa dhidi yake isipokua kama ofisa wa polisi anayehusika akiwa anaamini kwamba mtuhumiwa amefanya kosa kubwa."*

Pamoja na hayo, Sheria hiyo ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya mwaka 1985 inawataka polisi kuwapa watuhumiwa haki nyingi za msingi. Katika kifungu cha 53 pamoja na 54 cha sheria hiyo Polisi ana wajibu wa kumpa haki mtuhumiwa ikiwa ni pamoja na haki ya kuwasiliana na ndugu, jamaa au wakili wake. Pamoja na mambo mengine sheria hii inamtaka askari wa jeshi la polisi kumpa mtuhumiwa haki yake ya kupata msaada wa kisheria kutoka kwa wakili.

Pia kifungu cha 55 kinaeleza kwa kina jinsi ambavyo mtuhumiwa anapaswa kutendewa anapokua chini ya ulinzi wa polisi. Kifungu hicho kinaeleza kwa tafsiri isiyo rasmi kama ifuatavyo:

***55.-(1)*** *Pindi Mtu, anapokuwa kizuizini, atapewa nafasi ya kutibiwa na kutendewa kwa ubinadamu na utu (A person shall, while under restraint, be treated with humanity and with respect for human dignity).*

***(2)*** *Hakuna mtu ambaye, wakati yuko chini ya ulinzi atakayepewa adhabu za kikatili na zisizo za kibinadamu*

***(3)*** *Inapotokea mtuhumiwa aliyeko kizuizini-*

*(a) Anatoa ombi kwa Ofisa wa Jeshi la Polisi ili apewe matibabu, ushauri au msaada kuhusu ugonjwa au jeraha; au*

*(b) Anaenda kwa Ofisa wa Jeshi la Polisi kuomba matibabu, ushauri au msaada kuhusu ugonjwa au jeraha,*

*Ofisa huyo wa jeshi la Polisi atachukua hatua zinazostahili kuhakikisha kuwa mtuhumiwa huyo anapewa matibabu, ushauri au msaada.*

Ni jambo la kusikitisha kuona kuwa mara nyingi polisi wameshindwa kusimamia na kutekeleza kwa vitendo vipengele muhimu vilivyopo kwenye sheria zetu na kusimamia haki za mtuhumiwa wakati wa ukamataji na wakiwa mahabusu. Taarifa ya ufuatiliaji wa matukio ya ukatili (torture nchini) ya THRDC ya waka 2018 inaonyesha watuhumiwa wanafanyiwa ukatili mwingi wakati wa ukamataji, wakiwa vituoni na wakati wa mahojiano na polisi. Aina ya ukatili unaoongoza ni kipigo, kukaa njaa, kulazwa mahala pasipo na utu na vitisho vya maneno.

Matukio kama haya ya kuwaweka kizuizini watuhumiwa kwa muda mrefu yamekua yakijirudia nchi nzima. Mara kwa mara Jeshi la Polisi limekua likiwakamata watuhumiwa na kuwaweka kizuizini kwa muda mrefu na baadae kuwaachia huru baada ya kukosa sababu za kuendelea kuwaweka kizuizini au kuwaachia huru kutokana na amri ya mahakama.

Baadhi ya watuhumiwa waliowahi kukamatwa na kushikiliwa kwa muda mrefu na baadae kuachiwa ni pamoja na Abdul Nondo aliyeshikiliwa kwa takribani siku 15 kabla ya kupelekwa Mahakamani (Kuanzia tarehe 06 Machi hadi 21 Machi 2018), Mwanasheria na Mwanasiasa Hashim Rungwe alishikiliwa na Polisi kwa zaidi ya siku 4 mwaka 2017 bila kupelekwa Mahakamani.

Wengine ni mwanzilishi wa mtandao wa Jamii Forum Maxence Melo aliwahi kuwekwa kizuizini kwa siku nne kabla ya kupelekwa mahakamani, Wanasiasa Freeman Mbowe, Tundu Lisu, Ester Matiko na Joseph Mblinyi waliwahi kukamatwa katika mazingira tofauti na kuwekwa kizuizini kwa muda mrefu, Wakili Wilson Mafie alikamatwa na poilisi na kuweka katika kizuizi cha polisi kwa muda wa wiki moja mjini Dar es Salaam, Watetezi wa Haki za Binadamu Loliondo (Supuk Olemaoi na Clinton Mshao) walikamatwa na kuwekwa kizuizini kwa jumla ya siku 6, Ndugu Henry Nkya wa Mbeya alikamatwa na askari wa jeshi la polisi kwa tuhuma za kufanya makosa ya kimtandao na kuwekwa kwenye kizuizi kwa muda wa siku 15 hadi sasa.

Wakati mwingine vitendo hivi vya jeshi la polisi vimesababisha vifo vya watuhumiwa wanapokua katika vituo vya polisi. Kwa mfano Ndugu Chacha Heche Suguta (Mdogo wake mbunge John Heche) alifariki akiwa mikononi mwa polisi mwaka 2018 kutokana na kukiukwa taratibu za kisheria za kuwakamata na kuwaweka kizuizini watuhumiwa.

Hawa ni baadhi tu ya watu waliowahi kuwekwa kizuizini kwa muda mrefu kinyume na sheria na huku haki zao zingine za msingi zikivunjwa. Wapo raia wengine wengi waliowahi kushikiliwa na polisi kwa muda mrefu kabla ya kufikiswa Mahakamani au kuachiwa huru baadae kutokana na kukosa sababu za msingi za kuendelea kuwashikilia.

**Mwendelezo wa Ukiukwaji wa Haki za Binadamu Wilayani Ngorongoro-Loliondo**

Kumekua na mwendelezo wa ukiukwaji wa haki za binadamu Loliondo kwa muda mrefu sasa. Hii imetokana hasa na uwepo wa mgogoro wa ardhi kati ya wananchi wa Loliondo na mwekezaji, kampuni ya OBC ambayo imehodhi eneo kubwa. Mgogoro huo kwa kiasi kikubwa umeongeza ukiukwaji wa haki za binadamu huku Jeshi la Polisi wilayani humo pamoja na vyombo vingine vya usalama wa raia na wanyaama pori  vikihusika mara kwa mara kuwanyanyasa wananchi wa Loliondo. Operesheni mbalimbali pia zimekuwa zikichangia kwa kiasi kikubwa ukiukwaji wa haki za binadamu na watuhumiwa loliondo na kwingine nchini.

Kwa mfano mwaka 2017, Maofisa wa Jeshi la polisi walishiriki katika operesheni ya kuwaondoa wananchi katika vijiji 14 vya Loliondo. Mamia ya makazi ya wananchi na mali vilichomwa moto, watu walijeruhiwa vibaya huku wengine wakikamatwa na kuwekwa kizuizini kwa muda mrefu. Kwa mfano Kwa Ngorongoro kwa mwaka 2018 tu zaidi ya watu 100 wameshakamatwa katika opersheni hizi wakati mwingine bila sababu za msingi. Wengine wamepelekwa vituo vya polisi Mugumu Serengeti na Mwanza.

Vitendo vya kukamata raia na Watetezi wa Haki za Binadamu bila sababu za msingi, huku wakivunjiwa haki zao za msingi limekua ni jambo la kawaida. Mara kwa mara Maofisa wa Jeshi la Polisi Ngorongoro na washirika wao wamekua wakirudia vitendo vya kuwakamata raia na kuwaweka kizuizini na baadae kuwaachia.

Itakumbukwa kwamba tarehe 7 Januari 2019, Watetezi wawili wa Haki za Binadamu (Clinton Kairungi na Supuk Maoi) pamoja na raia wengine wawili walikamatwa na kuwekwa ndani kwa zaidi ya siku sita bila kupewa haki zao za msingi. Pia katika operesheni nyingine ya kutafuta silaha kwa wananchi Askari Polisi kwa ushirika na kikosi maalum cha operesheni hiyo Ngorongoro wamekuwa wakiwashikilia watu kwa muda mrefu kituoni. Mfano Aloyce Ngurumwa na watu wengine 13 walishikiliwa kuanzia tarehe 18 Januari 2019 hadi 21, January 2019, huku wakizuiwa kuonana na ndugu .

Katika tukio hili la kutisha la sasa ni watu watano wamefanyiwa ukatili na askari wa Loliondo na Ngorongoro. Wengi kwa sasa wamelazwa hopstalini kufanyiwa upasuaji wa miguu ili kuwatibu majeraha makubwa waliyonayo. Unyanyasi dhidi ya raia Ngorongoro ni jambo la kawaida sasa na hakuna hatua stahiki zinazochukuliwa. Watu hawa baadaye waliachiwa bila hata kushtakiwa kwa kosa lolote baada ya kukaa rumande kwa siku 15. Hii inamaanisha wananchi hawa walipaswa tu kuhojiwa bila kukamatwa kwa tukio hili la wizi achilia mbali mateso waliyoyapata,

Vitendo vya kupiga raia, kuwanyima PF3, kuwaweka mahabusu muda wanaojisikia polisi imekuwa jambo la kawaida huko Ngorongoro na maeneo mengine nchini. Taarifa hizi wanazo viongozi wa Wilaya kama Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Polisi Ngorongoro na Mkuu wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha lakini bado hakuna hatua zilizochukuliwa dhidi ya askari hawa.

**Madhara ya Polisi kuwaweka kizuizini watuhumiwa kwa muda mrefu**

Madhara ya polisi kuwaweka kizuizini watuhumiwa kwa muda mrefu kinyume na sheria ni makubwa sana na tumeshudia maeneo mengi ya Taifa. Madhara hayo ni;

i. Polisi hawana mafunzo rasmi ya kukaa na watuhumiwa rumande kwa muda mrefu kama ilivyo kwa askari magereza ambao wamefunzwa kuishi na wafungwa au watuhumiwa kwa muda mrefu.
ii. Polisi hawana rasilimali watu na mali kwa ajili ya kuwahudumia wafungwa wa muda mrefu chakula na vitu vingine muhimu vya kibadamu, hivyo hii hupelekea watuhumiwa kushinda njaa katika baadhi ya vituo hasa wale wanaokaa kwa muda mrefu kama hao watano wa Loliondo waliokaa siku 15, huku wakizuiwa kuonana na ndugu zao.
iii. Watuhumiwa wengi hupata mateso makubwa sana wakiwa rumande kwa muda mrefu kutokana na kwamba vyumba hivyo havina uwezo wa kubeba watuhumiwa wengi kwa wakati mmoja na kwa muda mrefu, vingine havina mfumo mzuri wa hewa na hali ya usafi kuwa duni hivyo kuchochea uwezekano wa kuambukizana magonjwa.
iv. Wengine huishia kupata majeraha na baadhi hata kupoteza maisha kutokana na ukatili na mazingira mabaya
v. Kwa kuwa Polisi hawana hata watoa huduma za afya kama ilivyo kwa magereza imekuwa vigumu kugundua matatizo ya kiafya kwa watuhumiwa wanaokaa zaidi ya siku mbili katika vituo.
vi. Kuchochea vitendo vya rushwa kwa jeshi la polisi kutoka kwa ndugu za watuhumiwa ambao hushawishika kutoa pesa ili ndugu zao waachiwe.

**Wito Wetu**

i. Tunaitaka Serikali na Uongozi wa Juu wa Jeshi la Polisi kuchukua hatua kali dhidi ya askari waliohusika na ukatili huu ambao ni kinyume na haki za binadamu kama zilivyoanishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na sheria za nchi. Pia Serikali igharamie matibabu ya wahanga hawa.

ii. Tunaendelea kulisisitiza jeshi la polisi kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi, ueledi na kuacha utaratibu wa sasa wa kukaa na watuhumiwa mahabusu zaidi ya siku moja.

iii. Tunavishauri vyombo vya usalama vilivyoko Loliondo, visimamie usalama wa raia eneo hilo na kuepuka kuingia katika kasumba ya muda mrefu ya kuwaonea jamii za kifugaji hasa wamasai wanaoishi eneo la Ngorongoro/Loliondo.

iv. Mkuu mpya wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha awawajibishe askari wote waliohusika na ukatili dhidi ya raia hawa watano wa Loliondo

v. Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania pamoja na Waziri wa Mambo ya Ndani waingilie kati swala hili la kuteswa kwa watuhumiwa huko Loliondo na maeneo mengine chini

vi. Endapo haya hayatafanyika hatua za kisheria zitafuata dhidi ya askari waliohusika na ukiukwaji huu mkubwa wa haki za raia.

vii. Tunawaomba watanzania wote, viongozi wa dini, viongozi wa serikali, vyama vya siasa, Waziri wa Mambo ya Ndani, waandishi wa habari na Asasi za Kiraia muunge mkono kampeni hii ya kupinga ukatili dhidi ya

watuhumiwa na wafungwa wanaokuwa rumande na magerezani nchini Tanzania(Tetea Haki za Mtuhumiwa).

viii. Kwa yoyote mwenye taarifa ya kuhusu kuteswa kwa watuhumiwa au kukaa muda mrefu vituoni piga namba (+255742322586 and +255755490360) pia tumia hashtag hii kuweka taarifa mtandaoni #TeteaHakizaMtuhimiwa

**Imetolewa leo tarehe 22 Januari 2019**

**Na,**

**……………………………………………………**
**Wakili Anna Henga**
**Mkurugenzi**
**Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)**

**……………………………………………………**
**Onesmo Olengurumwa**
**Mratibu wa Kitaifa**
**Mtandao wa Wateetzi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC)**